# HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA TANGA MHE. WAZIRI WAZIRI KINDAMBA KATIKA HAFLA YA UFUNGUZI WA KONGAMANO LA UWEKEZAJI NA UZINDUZI WA MWONGOZO WA FURSA ZA UWEKEZAJI MKOA WA TANGA 16/11/2023

- **Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muunano wa Tanzania,**
- **Waheshimiwa Mawaziri,**
- **Katibu Mkuu Kiongozi- Serikali ya Mapinduzi Zanzibar,**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa (Geita, Morogoro, Kilimanjaro, Pwani, Arusha na Manyara)**
- **Waheshimiwa Manaibu Mawaziri,**
- **Waheshimiwa Mabalozi,**
- **Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi,**
- **Makatibu Wakuu,**
- **Makatibu Tawala wa Mikoa (Tanga, Dar Es Salaam, Geita, Morogoro, Kilimanjaro, Pwani, Arusha na Manyara)**
- **Watendaji Wakuu – TPSF, CTI, TCCIA**
- **Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali,**
- **Kamati ya Usalama ya Mkoa,**
- **Makatibu Tawala wa Wilaya Mkoa wa Tanga,**
- **Wakurugenzi Mamlaka za Serikali za Mitaa Mkoa wa Tanga,**
- **Watumishi wa Umma,**
- **Wawakilishi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali,**
- **Wafanyabiashara na Wawekezaji wa ndani na nje ya Tanga,**

- **Viongozi wa dini,**
- **Wanahabari,**
- **Wageni waalikwa…mabibi na mabwana.**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Mhe. Waziri,**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na ukarimu kwa kutupa nafasi yakuweza kukutana kwa ajili ya uzinduzi wa kongamano hili.

Pia ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, kwa maono na miongozo yake ya kuliongoza Taifa hili. Aidha natoa shukrani na pongezi za dhati kwa wasaidizi wake wa karibu, **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** na kwako wewe **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**Mhe. Waziri,**

Nasimama mbele yenu kwa furaha na bashasha kubwa kwa kukutana kwa ajili ya Kongamano la Uwekezaji la Mkoa wa Tanga na Uzinduzi wa Mwongozo wa Fursa za Uwekezaji Mkoa wa Tanga. Tukio hili ni la kihistoria katika juhudi zetu za pamoja za kusukuma maendeleo ya kiuchumi ya Mkoa wa Tanga. Kaulimbiu ya Kongamano hili ni, ″**Wekeza Tanga kwa Uwekezaji Endelevu**″ ambayo inaeleza utayari wetu katika kuhakikisha tunavutia, kuwapokea na kuwalea wawekezaji wote walio tayari wa ndani na nje ya Nchi katika kuwekeza Mkoani Tanga.

**Mhe. Waziri,**

Mkoa wa Tanga, una faida za kipekee za kijiografia na umuhimu wa kihistoria, kwa muda mrefu Mkoa wa Tanga umekuwa mdau muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Mkoa wetu umejaaliwa kuwa na rasilimali mbalimbali, miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, reli, majini na njia ya anga hivyo kuufanya Mkoa huu kuwa rahisi kufikika. (Mkoa wa Kimkakati). Pamoja na ukuaji wa kiuchumi tulionao, bado kuna nafasi ya kukua zaidi. Serikali imekiri hili na inaweka jitihada za dhati na za makusudi kuufanya Mkoa wa Tanga kuwa Mkoa wenye nguvu zaidi kiuchumi.

**Mhe. Waziri,**

Dhamira ya kuboresha hali ya uchumi ya Mkoa wa Tanga inaonekana katika hatua za kina zinazotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuanzia uwekezaji mkubwa katika maendeleo ya miundombinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na maboresho makubwa ya bandari ya Tanga, barabara, nishati, kuunda sera zinazochochea ukuaji wa viwanda na uwekezaji na kuweka mazingira rafiki ya ukuaji wa biashara. Ufufuaji na uanzishwaji wa viwanda umekuwa kitovu si tu kwa ajili ya kuzalisha ajira bali pia kwa kurejesha Mkoa wa Tanga kama kitovu cha viwanda na biashara. Tunaboresha miundombinu na mazingira yote muhimu ili kuvutia wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

**Mhe. Waziri,**

Kongamano la Uwekezaji la Mkoa wa Tanga; ni mpango mkakati wa kuonesha, kuzielezea na kuzitangaza fursa zote za kiuchumi zilizopo Mkoani Tanga. Tunaamini katika nguvu ya majadiliano na ushirikiano, Kongamano hili litatumika kama daraja kati ya wawekezaji watarajiwa na fursa changamfu na adhimu zinazooneshwa hapa. Ni ushahidi wa

kujitoa kwetu kwa kuwashirikisha wadau wote kwa uwazi na maono ya pamoja katika maendeleo ya uchumi wa Mkoa wa Tanga.

**Mhe. Waziri,**

Tumekuwa na mawasiliano na ushirikiano ya karibu na Waheshimiwa Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania katika mataifa mengine lakini pia wale wanaowakilisha mataifa mengine hapa kwetu Tanzania. Tunafahamu namna ambavyo wana jukumu muhimu kama wanadiplomasia na tunatambua ushawishi wao katika kujenga mitazamo ya kimataifa ya namna ambavyo Tanzania inatazamwa katika muktadha wa kidunia. Tunawakaribisha kuungana nasi katika kutangaza Mkoa wa Tanga kama kivutio kikuu cha uwekezaji. Ushawishi wao, uhusiano wao wa kidiplomasia na uwezo wao wa kuwezesha ushirikiano ya kimataifa ni nguzo muhimu sana katika kuvutia wawekezaji ambao watachangia sio tu ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Tanga bali pia ushirikiano wa kimataifa.

**Mhe. Waziri,**

Wakuu wetu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wana mchango mkubwa katika kutafsiri Sera za kitaifa katika mipango tunayoitekeleza na tunayoitarajia kuitekeleza. Wao siyo tu ni wasimamizi bali pia ni watetezi wa fursa za ndani, uhusiano na wawekezaji watarajiwa, na walinzi wa utambulisho wa kipekee na uwezo wa Wilaya zao. Tunategemea uongozi wao na maarifa ya ndani kuunda mazingira ya kuvutia na yanayofaa kwa uwekezaji endelevu. Nikuhakikishie **Mhe. Waziri** na kuwahakikishia wawekezaji kuwa tumejipanga vizuri sana katika hili kuhakikisha dira na maono ya viongozi wetu wa juu zinatimia.

**Mhe. Waziri,**

Tunapotazama miaka kadhaa mbele, tunauona Mkoa wa Tanga utakaokua kinara wa maendeleo ya kiuchumi. Katika miaka mitano, tunatamani kushuhudia mandhari iliyo na viwanda vingi vinavyostawi, yenye shughuli nyingi za uchumi na biashara, na jamii inayofurahia faida za kuongezeka kwa nafasi za ajira. Maono yetu yanakwenda mbali zaidi ya ustawi wa kiuchumi; tunaiangalia Tanga ambayo inakua mfano wa maendeleo endelevu, yenye uwekezaji unaochangia sio tu ukuaji wa uchumi bali pia ustawi wa jamii. Hivyo wawekezaji watarajiwa wafahamu kuwa wana-Tanga wana kiu kubwa sana ya maendeleo na wapo tayari kuwapokea na kuwahakikishia mipango yao watakayojiwekea inatimia ambayo hatimae itatimiza ndoto za maendeleo ya kiuchumi ya Mkoa wa Tanga.

**Mhe. Waziri,**

Kwa kumalizia, natoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa wote waliopo hapa. Ushiriki wenu katika tukio hili ni uthibitisho wa dhamira yetu ya pamoja katika kutengeneza mustakabali wenye mafanikio. Tuanze safari hii kwa pamoja, kwa kutumia nguvu za Mkoa wa Tanga na moyo wa ushirikiano wa wadau wote waliopo, ili kutengeneza urithi wa kiuchumi utakaodumu kwa vizazi na vizazi.

***Ahsanteni kwa kunisikiliza.***